# AAP Nº 47

# SWAHILI FORUM III

Edited by Rose-Marie Beck, Thomas Geider, Werner Graebner

SEPT 1996

SWAHILI FORUM III

**Edited by**
**Rose-Marie Beck**
**Thomas Geider**
**Werner Graebner**

Afrikanistische Arbeitspapiere
Institut für Afrikanistik
Universität zu Köln
50923 Köln
Germany

Cover design: Donald A. Lessau / R.-M. Beck / Th Geider

©, by the editors

**ISSN 0178-725X**

*AAP 47 (1996): 63-71*

# *Uo mmoja hautiwi panga mbili:* AINA ZA YAMBWA NA MAANA ZAKE

THILO C. SCHADEBERG

"Kinds of objects and their meanings" deals with objecthood in Kiswahili. From a syntactic point of view, there is but one kind of object: the distinction between "direct" and "indirect" object has no syntactic properties, and one verb can have only one object. Of course, objects can have different semantic roles. This raises questions about the syntactic and semantic functions of "naked" non-objects, and some of these are approached by inspecting fifty examples of the verb *kutia* 'to put [sth] [into]' from Sacleux's dictionary. Three syntactic and semantic frames are distinguished and the respective roles of the arguments are described. Finally, there is a brief discussion about the meaning of the object as such and how it is influenced by the presence of the applicative extension.

## 1. Yambwa na yambiwa?

*Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (KSIL) inaeleza sehemu kuu za sentensi (yaani, kwa Kiingereza, *subject, object, direct object, indirect object)* kama ifuatavyo:

(1) **Kiima:** sehemu ya kwanza ya tungo ambayo huelezwa na kiarifu (katika mgao wa uwili wa sentensi).
**Yambwa:** neno linaloashiria kitendwa au kitendewa katika sentensi.
**Yambwa tendwa:** nomino yenye kuashiria kitendwa katika sentensi.
**Yambwa tendewa:** neno lenye kuashiria kitendewa katika sentensi.

Siku hizi, ninavyoelezwa na Dkt K. Kahigi (mawasiliano ya binafsi), *yambwa tendwa* na *yambwa tendewa* huitwa pia *yambwa* na *yambiwa.*

Maelezo ya KSIL hayafai kabisa kwa sababu yanachanganya viwango vya sintaksia na vile vya semantiki na usemi. (Kiwango cha tatu, yaani kiwango cha usemi, sitakiangalia sana katika makala haya.) Tukisema kiima ni "sehemu ya kwanza ya tungo ambayo huelezwa na kiarifu" basi tuko kwenye kiwango cha usemi. Ingawa mara nyingi kiima ni mada na kiarifu ni maelezo, pengine utaratibu wa sentensi si hivyo. Angalia sentensi hii:

(2) *Mikono yake aliizamisha mifukoni na macho yake akayatupa mbele kwenye upeo.* (Bearth 1995:189)

Katika sentensi hii *mikono yake* na *macho yake* yako mwanzoni mwa tungo na kuelezwa na maneno yanayofuata. Lakini si viima, bali ni yambwa. (KSIL inatumia istilahi *kiarifu* kwa kutafsiri Kiingereza *predicate* ambayo ni kazi ya kisintaksia na pia *comment* ambayo ni kazi ya

kisemantiki.) Vilevile, tukisema yambwa ni kitendwa au kitendewa, basi tuko kwenye kiwango cha semantiki.

Tukitaka kuchambua sentensi kisintaksia, lazima tutumie vigezo vya kisintaksia pamoja na vya kimofolojia. Haya tujaribu:

(3) Katika lugha ya Kiswahili, **kiima** ni sehemu ya sentensi ambayo inamiliki upatanisho wa kiambishi-kiima katika kitenzi-arifu.

Kisemantiki, kiima bora ni kitenda, lakini pengine chaweza kuwa ni kitendwa, kitendewa, na hata mahali n.k. (Natumia istilahi *kitenda, kitendwa* na *kitendewa* hasa kama ni watu.)

(4) *Wavuvi wa-me-kamata samaki.*
*Samaki wa-na-patikana sokoni.*
*Samaki wa-na-uzwa sokoni.*
*Watu wa-na-uziwa samaki sokoni.*
*Sokoni ku-na-patikana samaki.*

**Yambwa** ina sifa zifuatazo katika lugha ya Kiswahili:

- Yambwa inaweza kumiliki upatanisho wa kiambishi-yambwa katika kitenzi-arifu.
- Mojawapo ya viambishi-yambwa ni kiambishi-jirejee.
- Tukiwa na sentensi yenye yambwa tunaweza kuzalisha sentensi nyingine kwa njia ya kunyambua kitenzi kikawa katika umbo la kutendwa. Katika sentensi hii mpya, yambwa ya asili imekuwa ni kiima (chenye sifa zake za kisintaksia).
- Mahali bora pa yambwa, katika tungo la sentensi, ni kufuata kitenzi-arifu moja kwa moja.

Kisemantiki, yambwa bora ni kitendwa, lakini pengine ina maana nyingine, hasa maana ya kitendewa. Kisintaksia, yambwa-tendwa na yambwa-tendewa zina sifa zile zile.

(5) *Wa-li-m-kamata mwizi.*
*Wa-li-m-kamatia mzee samaki.*

Katika sentensi ya kwanza, *mwizi* ni yambwa-tendwa, katika sentensi ya pili, *mzee* ni yambwa-tendewa. Zote mbili zinatokea katika kitenzi kama kiambishi-yambwa, yaani *-m-*. Tunaona tena kwamba yambwa *mzee* inatangulia neno *samaki,* na hivyo ni tungo la sentensi la kawaidia. Lakini pengine tunaweza kukuta tungo jingine:

*A-li-wa-fungulia mlango wanyama.* (Barwani Sheikh 1995:13).

Sasa tuangalie kiambishi-jirejee *-ji-*.

(6) *Samaki wa-li-ji-kamata.*
*Wavuvi wa-li-ji-kamatia samaki.*
*$ Samaki wa-li-ji-kamatia wavuvi.*

Katika sentensi ya kwanza, *samaki* ni mtenda na pia ni mtendwa. Katika sentensi ya pili *wavuvi* ni watenda na pia ni watendewa. Sentensi ya tatu ni sawa ikiwa waliokamatwa ni wavuvi, lakini sentensi haiwezi kutoa maana kuwa 'samaki walijikamata wenyewe kwa ajili ya wavuvi'.

(7) *Mwizi a-li-kamat-w-a (na askari polisi).*
*Mzee a-li-kamat-i-w-a samaki (na wavuvi).*
*$ Samaki wa-li-kamat-i-w-a mzee.*

Katika sentensi ya kwanza, kiima kipya, yaani *mwizi,* kina maana ya mtendwa, na katika sentensi ya pili, kiima kipya, yaani *mzee,* kina maana ya mtendewa. Sentensi ya tatu ni sawa ukitaka kusema kwamba mzee alikamatwa kwa ajili ya samaki, lakini haiwezi kutoa maana kwamba samaki walikamatwa kwa ajili ya mzee.

Basi, ikiwa hatuwezi kutofautisha kisintaksia baina ya yambwa-tendwa na yambwa-tendewa, inatubidi kuziita zote mbili yambwa. Kutoka sasa, nitatumia istilahi *yambwa-tendwa* kuwa na maana ya 'yambwa yenye maana ya kitendwa' na *yambwa-tendewa* kuwa na maana ya 'yambwa yenye maana ya kitendewa'. Lakini kisintaksia, zote mbili ni yambwa tu, basi.

Sasa, tuangalie tena sentensi hizi:

(8) *Wa-li-m-pa mzee zawadi.*
*Wa-li-mw-eleza mzee shida yao.*

Ni dhahiri kwamba, *mzee* ni yambwa katika sentensi hizo. Lakini, hatujaeleza kazi ya kisintaksia ya *zawadi* na *shida yao* katika sentensi hizo. Wengine huchambua sentensi za aina hiyo kama ni sentensi zenye yambwa mbili, yaani yambwa ya kwanza na yambwa ya pili (Y1, Y2; taz. Dryer 1986):

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (9) | *Wa-li-m-pa* | *mzee* | *zawadi.* | |
| | | mtendewa | kitendwa | (kiwango cha semantiki) |
| | | Y1 | Y2 (?) | (kiwango cha sintaksia) |
| | *Wa-li-i-toa* | *zawadi.* | | |
| | | kitendwa | | |
| | | Y1 | | |

Sasa tujiulize: Sifa za Y2 ni zipi? Kwa kweli, mimi sijui. Ni rahisi kutofautisha baina ya Y2 na Y1 kwa vile Y2 haina sifa zozote za Y1. Lakini si rahisi kabisa kutofautisha Y2 na sehemu nyingine za sentensi zinazofanya kazi za vielezi, au CHAGIZO. (Nitatumia istilahi *kielezi* kama ni kazi ya kisintaksia, si kama aina ya maneno.)

Kutokuwa na kihusishi (PREPOSITION) si sifa maalum ya yambwa. Kwa Kiingereza, katika *he gave her a present,* Y2 (yaani *present* 'zawadi') inatofautishwa na vielezi vingine kwa

kukosa kihusishi. Lakini, katika lugha ya Kiswahili vielezi vingi havina kihusishi bali ni (makundi ya) nomino tupu.

| | | |
|---|---|---|
| (10) | *Waliondoka upesi.* | *$ Upesi uliondokwa.* |
| | *Waliondoka haraka.* | *$ Haraka iliondokwa.* |
| | *Waliondoka kimya.* | *$ Kimya kiliondokwa.* |
| | *Wamekaa chali.* | *$ Chali kimekaliwa.* |
| | *Wamevaa kienyeji.* | *$ Kienyeji kimevaliwa.* |
| | *Walihama mwaka jana.* | *$ Mwaka jana umehamwa.* |
| | *Walihama mjini.* | *Mjini kumehamwa. [!]* |

Basi, tukishindwa kutambua sifa za yambwa ya pili (Y2), inatubidi kusema kwamba lugha ya Kiswahili ina yambwa moja tu. Kwa hiyo, tukiangalia tena sentensi za (8), inatubidi kusema kwamba *zawadi* na *shida yao* vinafanana na vielezi, au chagizo, yaani havina uhusiano maalum na kitenzi-arifu. Kisintaksia, tungeweza kusema vinaongeza habari juu ya mzee alivyopewa na kuelezwa.

## 2. Kutia

Kuna baadhi ya vitenzi ambavyo vinaleta shida kwa uchambuzi wangu kwa vile huonekana kuwa na yambwa mbili. Katika sehemu ifuatayo, nitatazama kitenzi kimoja cha aina hii, yaani kitenzi *kutia.*

Kamusi bora ya Kiswahili, yaani kamusi ya Sacleux (1939), inatoa mifano hamsini ya matumizi ya kitenzi *kutia* (taz. NYONGEZA). Tukitazama mifano hii, tunaweza kutofautisha mipangilio mitatu ya kisintaksia:

(11) i *kutia alama* (S4)
ii *kumtia mtoto chuoni* (S18)
iii *kumtia mtu adabu* (S24)

Katika mpangilio wa kwanza kitenzi kinafuatwa na kundi nomino moja. Kisintaksia, kundi hilo ni yambwa. Tungeweza kusema:

(12) *Alama hii imetiwa mwaka jana.*

Maana ya yambwa hiyo ni 'kitu kinachowekwa'. Tutaiita maana hii "MADA".

Katika mpangilio wa pili kitenzi kinafuatwa na makundi nomino mawili. Katika mfano wetu, nomino ya kwanza, yaani *mtoto,* ni yambwa. Tunaona kiambishi-yambwa *-m-* katika kitenzi, tena tungeweza kusema:

(13) *Mtoto ametiwa chuoni.*

Maana ya yambwa ni ile ile ya 'kitu kinachowekwa' au MADA. Nomino nyingine, yaani *chuoni,* ina kiambishi-tamati cha mahali *-ni.* Maana yake ni 'mahali pa kuwekea' au LENGO.

Katika mpangilio wa tatu kitenzi kinafuatwa na makundi nomino mawili vilevile. Nomino ya kwanza, ambayo ni *mtu* katika mfano wetu, ni yambwa kwa sababu tuna kiambishi-yambwa *-m-* katika kitenzi. Maana yake inafanana sana na maana ya 'mahali pa kuwekea' au LENGO, lakini tutaona baadaye kuwa iko tofauti ndogo. Nomino ya pili ambayo ni *adabu* katika mfano wetu ina maana ya 'kitu kinachowekwa', yaani MADA.

Kwa hiyo, tunaweza kutofautisha mipangilio mitatu hii:

| (14) | | YAMBWA | CHAGIZO |
|---|---|---|---|
| i | *kutia* | MADA | |
| ii | *kutia* | MADA | LENGO |
| iii | *kutia* | LENGO | MADA |

Mpangilio wa kwanza unafanana na wa pili kwa vile MADA ni yambwa. Lengo halitajwi katika mpangilio wa kwanza kwa sababu si muhimu. Tukisema *wametia nanga,* basi tunajua nanga imetiwa katika maji lakini mahali pake maalum hatutaki kujua; jambo lililo muhimu ni kwamba jahazi limefungwa.

Katika mpangilio wa pili LENGO linaweza kuwa ni nomino ya ngeli ya mahali yenye kiambishi-tamati *-ni* au linaweza kuwa ni kundi la kinomino kama *ndani ya kitu fulani, katika kitu fulani,* n.k.

(15) *kutia maji mtungini*
*kutia maji katika chupa* (S2)
*kutia maji ndani ya chupa* (S2)

Sasa tulinganishe mpangilio wa pili na mpangilio wa tatu. Yote miwili ina sehemu zile zile, yaani MADA na LENGO. Kisintaksia, tofauti baina ya mipangilio hii ni ipi ni yambwa. Tunaweza kuuliza, tofauti hii ya kisintaksia ina maana gani? Au, kwa maneno mengine, yambwa ina maana gani na chagizo kina maana gani.

Napendekeza kuwa yambwa ni kitu ambacho ni karibu zaidi na maana ya kitendwa kuliko makundi nomino mengine katika sentensi. Chagizo kinaeleza mambo mengine, kwa mfano mahali pa tukio fulani.

Tulinganishe sentensi hizi mbili:

(16) a. *Tia maji chupani.*
b. *Chupa itie maji.* (S2)

Katika sentensi hizi mbili, *maji* ni MADA, na *chupa* ni LENGO. Lakini, *chupa* ni mahali tu pa kuwekea maji katika (16a), lakini katika (16b) *chupa* ni kitendwa, yaani kitu kinacho-

badilishwa. Tunaona vilevile kwamba neno *chupa* lina kiambishi-tamati cha mahali *-ni* katika (16a) ambapo lina maana ya LENGO tupu tu, bali halina kiambishi hicho katika (16b) ambapo ni yambwa-kitendwa.

Sasa tunaweza kufahamu mifano ya mnyambuliko wa kutendwa. Tukitumia mnyambuliko huu tunajua kabisa kwamba kiima ni kitendwa.

(17) a. *kutiwa motoni* (S39) :: *kutia [kitu] motoni* (S17)
b. *Vyakula vimetiwa sumu* (S40) :: *kutia vyakula sumu*

Mifano ya (18) ni migumu kidogo. Katika *kutia motoni* (18a), neno *motoni* ni LENGO, yaani ni mahali pa kuwekea. Lakini, katika *kutia moto* (18b), neno *moto* ni MADA, yaani ni kitu kinachowekwa mahali fulani. Kwa hiyo, jozi hii ya sentensi haifanani na jozi nyingine ya (16). Sentensi za (18) zote mbili ni za mpangilio wetu wa pili, yaani MADA + LENGO.

(18) a. *kutia barua motoni* (taz. S17)
b. *kutia moto nyumbani* (taz. S16)

Kwa hiyo, sentensi hizi mbili haziwezi kuwa "asili" ya sentensi (19) iliyo katika kauli ya kutendwa:

(19) *kutiwa moto* (S38) :: *kutia nyumba moto*

Kama LENGO ni mtu (au mnyama?), mpangilio wetu wa pili hautumiki. Kuna sababu mbili, yenye asili ya kisemantiki. Sababu ya kwanza inahusu mofolojia: hatuwezi kutumia kiambishi-tamati *-ni* pamoja na neno ambalo linaashiria mtu. Sababu ya pili inahusu sintaksia: katika Kiswahili, ukitia kitu fulani katika mtu, k.m. hofu au adabu, basi mtu atafikiriwa kama yeye ni kitendwa, kitu kinamtokea, anabadilishwa. Kwa hiyo, mtu atapata nafasi ya kisintaksia ya yambwa, yaani, tunatumia mpangilio wa tatu. Sacleux anatoa mifano mingi:

(20) *kumtia mtu aibu* (S25)
*umetutia matata* (S5)
*kujitia ugonjwa* (S37)

Kila tukimkuta mtu katika mpangilio wetu wa pili, tunajua kwamba mtu huyu ni MADA, si LENGO.

(21) *kumtia mtoto chuoni* (S18)
*kumtia mtu kazini* (S32)

Basi, tumeona kwamba kitenzi *kutia* kinapokea yambwa za aina mbili: MADA au LENGO. Lakini hii si kusema kwamba sentensi kama *umetutia matata* ina yambwa mbili. Kuna mipangilio zaidi ya mmoja, lakini kila mpangilio una yambwa moja tu.

Inaonekana tena kwamba yambwa ya kawaida au yambwa ya asili ya kitenzi *kutia* iwe ni MADA. Tunatumia mpangilio wa tatu, yaani mpangilio ambao unatumia LENGO kama

**NYONGEZA**

Mifano ya matumizi ya kitenzi *kutia*, kutoka kamusi ya Sacleux (1939):

**-Tia** (S. G. *-chia*). a. Mettre, placer (*-weka*); mettre à, insérer, appliquer (à).

(S1) *-tia mafuta*, mettre de l'huile ou de la graisse (dans, à, sur), huiler, graisser.
(S2) *-tia maji*, mettre de l'eau (dans, à, sur), humecter, arroser.
(S3) *Tia maji katika (ndani ya) chupa*, mets de l'eau dans la bouteille : on dirait aussi *chupa itie maji*.
(S4) *-tia alama*, mettre une marque (à, sur), marquer
(S5) *Umetutia matata*, tu nous a mis dans l'embarras.
(S6) *-tia dawa*, appliquer un médicament (à).
(S7) *Tia hayo moyoni mwako*, mets cela dans ton entendement, dans ta mémoire.
(S8) *-tia rangi*, appliquer une couleur, colorer, badigeonner, peindre.
(S9) *-tia katika hisabu*, mettre en compte, sur le compte.
(S10) *-tia ugonjwa*, produire la maladie, infecter.
(S11) *-tia usingizi*, provoquer le sommeil, endormir, stupéfier.
(S12) *-tia giza*, produire l'obscurité, obscurcir.
(S13) *Kisu kukitia makali*, affiler (aiguiser) un couteau.
(S14) *-tia ufa*, faire une fente (à), fêler.
(S15) *-tia mkono*, mettre la main (à), donner un coup de main, mettre sa griffe (signature à).
(S16) *-tia moto*, mettre le feu (à).
(S17) *-tia motoni*, mettre au feu, sur le feu.
(S18) *-mtia mtoto chuoni*, mettre un enfant à l'école.
(S19) *-mtia mtoto mabakora*, appliquer à un enfant des coups de canne.
(S20) *-tia duka*, établir (ouvrir) une boutique.
(S21) *-tia nanga*, jeter l'ancre.
(S22) *-tia roho yake katika safari*, risquer sa vie (sa tête) dans une voyage.
(S23) *-tia nguvu*, faire violence (à qqn, *-mtia nguvu*), violenter, fortifier, mettre de l'énergie à faire qqch.
(S24) *-mtia mtu adabu*, donner de l'éducation à qqn, le civiliser; en mauvaise part, lui apprendre à vivre, le reprendre, le corriger (par la parole ou par un châtiment).
(S25) *-mtia aibu*, lui infliger un affront, lui faire honte, le déshonorer.
(S26) *-mtia hofu*, lui faire peur.
(S27) *-mtia hasira*, le mettre en colère.
(S28) *-mtia hila (toa)*, lui attribuer (imputer) un défaut (qu'il n'a pas).
(S29) *-mtia hasara*, lui causer du dommage.
(S30) *-mtia moyo*, lui donner du coeur, l'encourager.

yambwa, tunapotaka kueleza kwamba LENGO si lengo tu, bali ni kitendwa vilevile. Lakini sasa tuulize swali lingine: Kwa nini hatutumii mnyambuliko wa kutendea. Kazi maalum ya mnyambuliko huo ni kueleza kwamba hali ya neno fulani imebadilika na sasa neno hilo limegeuka kuwa yambwa. Hilo naona ni swali gumu, lakini nitajaribu kulijibu.

Yambwa ya kitenzi cha mnyambuliko wa kutendea ina maana ambayo si kitendwa halisi. Tazama sentensi hizo:

(22) a. Walinizungumza.
b. Walinizungumzia habari zake.

Kiambishi-yambwa ni *-ni-*, yaani 'mimi'. Katika (22a), mimi ni kitendwa, kweli, na sifa yangu imehasirishwa. Katika (22b), mimi ni mpokeaji wa habari fulani. Kwa hiyo, tuseme maana ya yambwa ya kitenzi cha mnyambuliko wa kutendea hasa ni MPEWA. Kwa hiyo, mnyambuliko huo hauelezi vizuri maana ya kitendwa. Kitenzi *kutia* kinapotumiwa katika umbo la kutendea, yaani *kutilia,* mara nyingi namba ya wachezaji katika sentensi imeongezeka:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (23) | a. | -MPEWA- | MADA | LENGO | |
| | | *M-tilie* | *kitambaa* | *chini ya sahani yake.* | (S45) |
| | | *U-si-m-tilie* | *moto* | *nyumbani.* | (S46) |
| | | *Ka-m-tilia* | *nguo yake* | *topeni.* | (S47) |
| | b. | -MPEWA- | LENGO | MADA | |
| | | *A-ka-ni-tilia* | *mwanangu* | *ndui.* | (S49) |

Mwisho, tuangalie jozi moja ya mifano mingine:

(24) a. *kumtia hofu* (S26)
b. *Usimtilie hofu* (S48)

Je, kuna tofauti gani baina ya mifano hii? Sacleux anatafsiri sentensi hizo zote mbili kama 'faire peur', yaani 'kuogofya'. Tunakubaliana naye kuhusu (24a); tulivyochambua sentensi hiyo mtu ambaye ni yambwa ni LENGO-kitendwa. Lakini maana ya (24b) ni tofauti. Alivyonieleza Dkt Y. Kihore (mawasiliano ya binafsi), sentensi hii inanfanana na *usimtilie mashaka,* yenye maana ya 'usimtuhumu' au 'usimwogope sana yule mtu', yaani "usiweke hofu na mtu huyu mahali pamoja". Hicho si Kiswahili safi, lakini maelezo hayo yanaweza kutusaidia kufahamu muundo wa (24b). Mtu ambaye ni yambwa si kitendwa, bali ni MPEWA; tena mtu ni LENGO na hofu ni MADA. Sentensi (24b) inafanana na (23b) isipokuwa LENGO na MPEWA vinahusu mtu yule yule. Sentensi (24b) inafuata mpangilio wetu wa tatu. Mnyambuliko wa kutendea unaeleza kwamba mtu huyu haingiwi na hofu (si kitendwa), bali anapata mahali pamoja na hofu.

(S31) *Tia moyo wako katika kazi hiyo,* mets ton âme (ton attention, ton application) à ce travail.

(S32) *-mtia mtu kazini,* mettre qqn au (à un) travail.

(S33) *-mtia utumwani,* le reduire à l'esclavage.

(S34) *-mtia uaskari,* l'enrôle dans la milice.

(S35) *-jitia haki,* se donner un brevet de probité.

(S36) *-jitia ukuu,* se mettre dans les grandeurs, y prétendre.

(S37) *-jitia ugonjwa* se prétendre malade.

(S38) *-tiwa moto,* être mis en feu.

(S39) *-tiwa motoni,* être mis au (dans, sur le) feu.

(S40) *Vyakula vimetiwa sumu,* les aliments sont empoisonnés.

(S41) Prov.: *Uo mmoja hautiwi panga mbili,* un seul fourreau ne peut recevoir deux sabres.

(S42) *Watoto walitiana mchanga machoni,* les enfants s'étaient mis (jeté) du sable dans les yeux.

(S43) *Wakatiana vigongo,* ils s'appliquèrent des coups de triques.

(S44) *Mfuko wa kutilia fedha,* bourse, porte-monnaie.

(S45) *Mtilie kitambaa chini ya sahani yake,* mets-lui une serviette sous son assiette.

(S46) *Usimtilie moto nyumbani,* ne lui mets pas le feu à la maison.

(S47) *Kamtilia nguo yake topeni,* il lui mit son linge (habit) dans la boue.

(S48) *Usimtilie hofu,* ne lui fais pas peur.

(S49) *Akanitilia mwanangu ndui,* il communqua la variole à mon enfant.

(S50) *Wajitiliani maneno haya? Si yako,* pourquoi te mêles-tu cela? Ce n'est pas ton affaire.

## MAREJEO

Barwani Sheikh, Sauda. 1995. Masomo ya bidii: a Swahili intensive course. Hamburg: Helmut Buske.

Bearth, Thomas. 1995. Wortstellung, Topik und Fokus. Katika *Swahili-Handbuch,* wahariri G. Miehe na W. J. G. Möhlig, k. 173–205. Cologne: Rüdiger Köppe.

Dryer, Matthew S. 1986. Primary objects, secondary objects and antidative. Language 62:808-845.

Sacleux, Charles. 1939. Dictionnaire swahili-français. (Travaux et mémoires de l'Institut de l'Ethnologie, 36-37.) Paris: Musée de l'Homme.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. 1990. *Kamusi sanifu ya isimu na lugha.* Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors kwa niaba ya TUKI.